# MTANDAO WA KUZUIA UKATILI WA KIJINSIAG

**Siku 16 za Unaharakati Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia 2017**

**Mapitio ya kampeni.**

# KILA MSICHANA ANA THAMANI!

JE! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

## KAULI MBIU:

## KILA MSICHANA ANA THAMANI! JE ! UTACHUKUA HATUA GANI ILI KUWAWEZESHA WASICHANA KUBAKI SHULENI?

Kila mwaka, kwa kipindi cha robo karne, wanaharakati ulimwenguni kote wamekuwa wakifanya kampeni wakati wa siku 16 za unaharakati kwa kuleta suala la Ukatili Dhidi ya wanawake (VAW) kama ajenda. kampeni hizi zimekuwa muhimu katika kuongeza ufahamu juu ya Ukatili Dhidi ya wanawake na kuainisha kazi ambazo zinahitajika kufanywa. Tathimini ya Kituo cha Uongozi wa wanawake ulimwenguni ya 2016 (CWGL) inaonyesha kuwa kampeni itafungua sura mpya duniani kote. CWGL imejidhatiti kubadili mwelekeo wa kampeni 'kutoka kwenye kuongeza uelewa kuelekea kwenye Kutokomeza' Ukatili wa kijinsia kwenye awamu ijayo ya Siku 16. Dhamira hii ina maana ya kuleta mabadiliko makubwa kwa kuchukua hatua zaidi na siyo kufanya masuala na kazi inayotakiwa kufanyika ionekane. Kampeni za siku za usoni zitawajibika kuingiza masuala muhimu ya haki za binadamu na uratibu bora kati ya mashirika yanayoshiriki na wadau.

Mwaka huu kampeni ya kimataifa itaendelea kuzingatia haki ya elimu kwenye mazingira ya vita, amani na mifumo mbalimbali ya elimu. Itakuwa ni kiunganishi kati ya ukatili wa kijinsia unaoambatana na mfumo dume na kutokuwepo usawa unaosababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya mamlaka

Katika ngazi ya kanda wanachama wa Mtandao wa Kuzuia ukatili wamekuwa wakishiriki katika kampeni tangu mwaka 2004. Mwaka huu, kulingana na kampeni ya kimataifa ya Kuzuia ukatili.Mtandao utazingatia katika kuhakikisha wasichana wanabaki shuleni. Utaainisha ubaguzi wa kimfumo kwa wasichana katika nyanja ya elimu kwa kuanzia nyumbani, mazingira ya shule, na sera za serikali zinazo athiri wasichana kupata elimu na utaalam. Kampeni italenga katika juhudi za kimataifa ili kuhakikisha elimu jumuishi yenye ubora na usawa kama ilivyoainishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu na.4. (ii)Pamoja na ahadi za serikali za Afrika zilizomo Kusini mwa Jangwa la Sahara ya kuhakikisha elimu ya msingi kwa wote.

Ingawa elimu ni haki ya msingi ya binadamu na serikali zimeahidi kutoa elimu ya bure na ya lazima kwa wote, wasichana bado wanakabiliana na vikwazo katika kuendelea na elimu ya juu. Katika nchi za Afrika zilizomo Kusini mwa Jangwa la Sahara, wasichana milioni 9 hawatahudhuria shule ikilinganishwa na wavulana milioni 6. Kwa ujumla, watoto milioni 34 wenye umri wa miaka 6 na 11 hawako shuleni katika ukanda huu. Moja ya Tatu ya watoto hawa wataanza katika umri mkubwa, lakini karibu nusu wataendelea kutengwa, na wasichana wanakabiliwa na vikwazo vikubwa. (iii)Ndoa za utotoni, mimba katika umri mdogo na sera / kanuni za kijamii ambazo zinazuia wasichana wajawazito kurudi shule, unyanyasaji na ubakaji, ni baadhi ya vikwazo vikuu.

- Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, asilimia 40 ya wanawake wanatumbukia kwenye ndoa za utotoni. (Iv) Mara kwa mara wasichana wanatolewa shuleni na kuolewa, mara nyingi kwa manufaa yatokanayo na mahari kubwa inayatolewa.

- Kufukuzwa wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shule imebaki kuwa ni sera ya kawaida katika nchi nyingi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara. Wasichana wananyimwa fursa ya kujiandikisha tena na kurudi shule mara baada ya kujifungua, bila kujali ni kwa kiasi gani wanajitahidi kuendelea na elimu; lakini kuna matukio mengi ya ubakaji / kulazimishwa kufanya ngono na kusababisha mimba. Kila mwaka, wasichana zaidi ya 8,000 nchini Tanzania wanatoka shuleni kwa sababu ya ujauzito. Wasichana walioolewa pia hufukuzwa shuleni. (V).
- Wasichana wanakabiliwa na unyanyasaji wa kingono, kudhalilishwa na kutwezwa nk. Haya yanaweza kufanywa na wageni au watu wasimamizi mashuleni (walimu, wafanyakazi, wanafunzi wenzao). Shirika la Human Rights Watch (Afrika Kusini ) katika majimbo matatu waliotembelea, walibainisha matukio ya ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia kwa wasichana yaliofanywa na walimu na wanafunzi wa kiume . (vi).

Mbali na Ukatili, wasichana wanakabiliwa na vikwazo vingi. Katika mazingira ya nyumbani, kwa sababu ya majukumu yao ya kijamii wasichana wanatumia muda zaidi katika kazi za nyumbani na muda kidogo kwenye kujifunza na maandalizi ya kitaaluma. Kutokana na ripoti iliyotolewa na UNICEF kabla ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa kike mnamo Oktoba 11, wasichana kati ya umri wa miaka 5 na 14 hutumia muda wa zaidi ya asilimia 40, au zaidi ya masaa milioni 160 kwa siku, wakifanya kazi za nyumbani zisizo na malipo kama kuchota maji na kusenya kuni ikilinganishwa na wavulana wa umri kama wao.

`Msichana akikatizwa masomo yake, ni wazi kwamba ni ukiukwaji wa haki zake; na kushindwa kuheshimu ahadi zilizowekwa na jumuiya / serikali. Hii inachochea kutokokuwepo na uwiano sawa wa mamlaka hali ambao tayari ipo kati ya wanawake na wanaume; inashinikiza wasichana / wanawake kuwa katika hali duni. Na hii sio tu inaleta hasara kwa wasichana / wanawake bali ni hasara kwa jamii na mataifa. Ikiwa tutawawesha wasichana kukamilisha elimu zao; tutapunguza hatari ya kukabiliwa na vitendo vya unyanyasaji, kiwango cha vifo vya watoto wachanga na mama wajawazito, ongezeko la idadi ya watu; na kuhakikisha familia zilizoelimika na taifa kwa ujumla. Elimu ni silaha yenye nguvu zaidi ambayo unaweza kuitumia kubadilisha dunia (Nelson Mandela). Unaweza kufanya kitu cha kuwasaidia wasichana kubaki shuleni, je wewe utachukua hatua gani?.

## KAMPENI INACHOKIOMBA.

kampeni ya Mtandao wa Kuzuia ukatili itaendelea kuzingatia elimu ya wasichana na kuomba wanajamii , wazazi, , shule na watunga sera kuchukua hatua ili kuhakikisha kwamba fursa ya upatikanaji na kukamilisha elimu iwe wazi kwa wasichana na wanawake. Tunaainisha haki za wasichana kupata elimu na kuchambua njia mbadala zitakazokikisha kuwa wasichana wanaishi na kukamilisha elimu yao. Tunapo ainisha suala la kufanya elimu kuwa salama kwa wote, mashirika yanaweza kuchagua suala mojawapo kutoka kwenye masuala tuliyo ainisha hapo chini au mchanganyiko wa masuala ambayo yanasababisha vizuizi kwenye elimu ya wasichana katika jamii zao na kusisitiza hatua za utekelezaji wa suala husika.

1. Upatikanaji wa elimu: hakikisha wasichana wote wanajiandikisha shuleni na kubaki shuleni mpaka wanapomaliza elimu ya juu
    a. Je, wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanapata elimu sawa katika jamii yako?
        i. Idadi ikoje ya wanafunzi wa kiume na kike katika viwango tofauti vya elimu katika jamii yako? Je! Mabadiliko ya uwiano yanajitokeza katika viwango vya juu? Kwa nini?
        ii. Je, kuna sera ambazo zinabagua wasichana (yaani, kufukuzwa shuleni wasichana wajawazito, nk.)

b. Hata wakati wasichana wanapata fursa ya elimu je,wanaruhusiwa kukamilisha masomo? Kuna vikwazo gani katika kukamilisha elimu ya msichana? Kwa umri gani wasichana / wanawake wadogo katika jamii yako wanaolewa? Je! Wanaendelea na elimu yao baada ya ndoa?

2. Mfumo wa elimu – Toa changamoto kwenye mifumo inayohamasisha ubaguzi na kutokuwepo na uwiano sawa wa mamlaka unaowakabili wasichana. Hakikisha mitaala na vitabu vya mafunzo vinahimiza na kuonyesha usawa wa jinsia

   a. Je! Ni Maudhui gani yanayofundishwa mashuleni yanayochangia ubaguzi wa wasichana na wanawake wenye umri mdogo -? (Je shule zinapanda mbegu za kutokuwepo na uwiano sawa wa mamlaka? Je, zinaimarisha dhana ya kwamba wavulana ni muhimu zaidi kuliko wasichana?)

   b. Je! Wasichana na wanawake wenye umri mdogo wanahamasishwa kushiriki katika shughuli zote kama wenzao wa kiume?

***Siku 16 za unaharakati ni fursa ya kuleta mabadiliko chanya. Je, wewe unahusikaje?***

Center for Women's Global Leadership. (2016) A LIFE OF ITS OWN an Assessment of the 16 Days of Activism Against Gender-Based Violence Campaign.

Sustainable development goal 4: Ensure inclusive and equitable quality education and promote lifelong learning opportunities for all. Retrieved from https://sustainabledevelopment.un.org/sdg4

UNESCO Institute for Statistics (UIS) and the Global Education Monitoring (GEM) Report. (July 2016). Policy Paper. Leaving no one behind: How far on the way to universal primary and secondary education? http://unesdoc.unesco.org/images/0024/002452/245238E.pdf

Girls not brides Report. (2015). Ending child marriage in Africa. http://girlsnotbrides.theideabureau.netdna-cdn.com/wp-content/uploads/2015/02/Child-marriage-in-Africa-A-brief-by-Girls-Not-Brides.pdf

Human Rights Watch https://www.hrw.org/news/2017/04/12/girls-sake-tanzania-should-stop-abuse-bias-schools

Human Rights Watch. March 1, 2001. Scared at School Sexual Violence Against Girls in South African Schools

UNICEF. (October 7, 2016). Press release: girls spend 160 million more hours than boys doing household chores everyday